



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA NNE (OKTOBA - DESEMBA) 2021,
BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
April 2022**

Yaliyomo

Majedwali	ii
Orodha ya Vielelezo	iii
Viambatisho.....	iv
1.0 Utangulizi	1
1.1 Uchumi wa Dunia.....	1
1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara	1
1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.....	1
1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.....	2
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania	3
1.5.1 <i>Pato la Taifa, Robo ya Nne Mwaka 2021</i>	3
1.5.2 <i>Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Nne, Mwaka 2021</i>	4
1.5.3 <i>Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Kipindi cha Robo ya Nne, Mwaka 2021</i>	5
1.5.4 <i>Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Nne, Mwaka 2021</i>	5
2.0 Kiwango cha Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi	6
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi	6
2.1.1 <i>Mazao</i>	6
2.1.2 <i>Mifugo</i>	7
2.1.3 <i>Misitu</i>	7
2.1.4 <i>Uvuvi</i>	7
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe.....	8
2.3 Uzalishaji Viwandani	9
2.4 Umeme	9
2.5 Maji	10
2.6 Ujenzi	10
2.7 Biashara na Matengenezo.....	11
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo	11
2.9 Malazi na Huduma za Chakula	12
2.10 Habari na Mawasiliano.....	12
2.11 Fedha na Bima.....	13
2.12 Upangishaji Majengo	13
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi.....	14
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala.....	14
2.15 Utawala na Ulinzi	14
2.16 Elimu	15
2.17 Afya.....	15
2.18 Huduma Nyingine za Jamii	15
3.0 Hitimisho	16

Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2021	8
Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano Robo ya Nne, Mwaka 2019 – 2021.....	12

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Nne 2020 na 2021 ..2	
Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Nne Mwaka 2016 - 2021	3
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne Mwaka 2014 – 2021.....	4
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika	4
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Nne, Mwaka 2021	5
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo ya nne, Mwaka 2020 na 2021	6
Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2021.....	10
Kielelezo Na. 8: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trillioni), Robo ya nne, Mwaka 2016 – 2021 ..13	

Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni	17
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia	19
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	21
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) – Asilimia	23

1.0 Utangulizi

Taarifa za Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina na kinachoaminika za mwenendo wa uchumi zinazotumika kutathmini mabadiliko yanayotokea katika vipindi vifupi vifupi kwa ajili ya kutayarisha sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika Nchi.

1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya mwezi Januari 2022, ilionesha kuwa uchumi wa dunia ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 5.9 katika mwaka 2021 kama ilivyokuwa imekadiriwa mwezi Oktoba 2021. Kiwango cha ukuaji huu kiko chini kwa pointi za asilimia 0.1 ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6.0 ya mwezi Julai 2021. Wakati huo huo, ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2022 umekadiriwa kuwa asilimia 4.4 ukilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.9 kilichokuwa kimekadiriwa hapo awali. Makadirio ya ukuaji kwa kiwango cha chini yanatokana na makadirio hafifu ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea za Marekani pamoja na nchi zinazoibukia kiuchumi ikiwemo China. Hali hii imechagizwa na sababu kadhaa ikiwemo hatua zinazochukuliwa kuendelea kukabiliana na maambukizi ya UVIKO 19.

1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara


Makadirio ya ukuaji wa uchumi mionganoni mwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara yalionesha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji kwa asilimia 4.0 ambalo ni ongezeko la pointi za asilimia 0.3 ikilinganishwa na makadirio ya mwezi Oktoba 2021. Kwa sasa uchumi wa Afrika Kusini unakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 4.6 mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 6.4 mwaka 2020; na pia uchumi wa Nigeria unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.0 mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 1.8 mwaka 2020.

1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa makadirio ya mwezi Januari 2022, ukuaji wa uchumi katika Jumuiya mwaka 2021 unatarajiwa kuimarika hadi asilimia 4.0 ambayo ni sawa na ongezeko la pointi za asilimia 0.3 ukilinganishwa na makadirio ya mwezi Oktoba 2021. Ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa

Afrika kama vile Afrika kusini umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.2 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.5 kipindi kama hicho mwaka 2020. Wakati huo huo, uchumi wa nchi nyingine katika Jumuiya katika robo ya nne ya mwaka 2021 uliongezeka kwa viwango tofauti katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2020 kama ifuatavyo: Tanzania uchumi uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.9 kutoka asilimia 4.8; Msumbiji uchumi uliongezeka kwa asilimia 3.3 kutoka kiwango hasi cha asilimia 1.8; Shelisteli uchumi uliongezeka kwa asilimia 0.1 kutoka kiwango hasi cha asilimia 5.0; na Mauritius uchumi uliongezeka kwa asilimia 6.2 kutoka kiwango hasi cha asilimia 11.9.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Nne 2020 na 2021




Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2021

1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa uchumi katika robo ya nne ya mwaka 2021 zimeonesha kuendelea kuimariika kwa ukuaji wa uchumi. Katika kipindi hicho, uchumi wa Rwanda uliongezeka hadi asilimia 10.3 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 0.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 na uchumi wa Uganda uliongezeka hadi asilimia 5.2 kutoka kiwango hasi cha asilimia 0.4. Aidha, uchumi wa Tanzania uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.9 ukilinganishwa na asilimia 4.8 katika robo ya nne ya mwaka 2020. Nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hazijatoa

mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2021.

Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Nne Mwaka 2016 - 2021



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2021

1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania


Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa robo ya nne (Oktoba - Desemba) 2021 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka shughuli zote za uchumi nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *2008 System of National Accounts*. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwanzoni mwa mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka.

1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Nne Mwaka 2021

Katika robo ya nne ya mwaka 2021, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika liliongezeka hadi shilingi trilioni 43.4 kutoka shilingi trilioni 40.4 kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi shilingi trilioni 36.9 katika robo ya nne mwaka 2021 kutoka shilingi trilioni 35.2 kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ukuaji wa asilimia 4.9.

Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne Mwaka 2014 – 2021




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021

1.5.2 *Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Nne, Mwaka 2021*

Mchanganuo wa mchango katika Pato la Taifa kwa shughuli kuu za kiuchumi katika robo ya nne ya mwaka 2021 unaonesha shughuli za kiuchumi za msingi zilikuwa na mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa wa asilimia 39.4, zikifuatiwa na huduma (asilimia 37.7) na shughuli za kati (asilimia 22.9). Mchango wa shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kabla ya kujumuisha kodi.

Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021

1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Kipindi cha Robo ya Nne, Mwaka 2021

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021, shughuli ya huduma nyingine za jamii (inayojumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri) ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha ukuaji wa asilimia 11.7; ikifuatiwa na huduma za chakula na malazi (asilimia 11.3); uzalishaji na usambazaji wa umeme (asilimia 10.6); habari na mawasiliiano (asilimia 9.3); fedha na bima (asilimia 8.7); utawala na ulinzi (asilimia 7.4); na uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 7.0).

Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Nne, Mwaka 2021



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021

1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Nne, Mwaka 2021

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2021 ziliikuwa na mchango katika ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 4.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, shughuli zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa asilimia 4.9 ziliikuwa ni pamoja na: kilimo (asilimia 23.2), ujenzi (asilimia 12.5), biashara na matengenezo (asilimia 9.0); uzalishaji viwandani (asilimia 8.4), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 6.4); utawala na ulinzi (asilimia 5.8); na fedha na bima (asilimia 5.6).

2.0 Kiwango cha Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi

2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvu

Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama. Shughuli hizi zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine na wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.


Katika robo ya nne ya mwaka 2021, shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 5.3 kama ilivyokuwa katika mwaka 2020.

2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora; kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji na kuimarika kwa huduma za ugani.

Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo ya nne, Mwaka 2020 na 2021



Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021

Katika robo ya nne ya mwaka 2021, mazao yaliyokuwa na mchango mkubwa wa ukuaji yalikuwa ni pamoja na mahindi yaliyoongezeka kwa asilimia 3.1 kutoka tani milioni 3.3 mwaka 2020 hadi tani milioni 3.4 mwaka 2021; maharage na mikunde yaliongezeka kwa asilimia 6.3 kutoka tani elfu 396 mwaka 2020 hadi tani elfu 421 mwaka 2021; viazi vitamu viliongezeka kwa asilimia 6.6 kutoka tani elfu 152 mwaka 2020 hadi tani elfu 162 mwaka 2021; na Mpunga uliongezeka kwa asilimia 14.4 kutoka tani elfu 692 mwaka 2020 hadi tani elfu 771 kipindi kama hicho mwaka 2021.

2.1.2 *Mifugo*

Shughuli hii inahusika na ufugaji wa ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika robo ya nne ya mwaka 2021, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 kiwango sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo uliolenga kukidhi mahitaji ya bidhaa za mifugo kutokana na kuongezeka kwa wastani wa pato la mwananchi, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa lishe bora.

2.1.3 *Misitu*

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikuwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 6.4 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.9 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na hatua za Serikali za kusimamia uvunaji endelevu wa mazao ya misitu.

2.1.4 *Uvuvi*

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi iliongezeka kwa kiwango hasi cha asilimia 11.6 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 19.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji hasi wa shughuli ya uvuvi ulisababishwa na kuendelea kupungua kwa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika kama vile petroli au gesi kama vile gesi asilia. Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi na ukusanyaji wa madini juu ya ardhi au kwenye visima. Shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha ni sehemu ya shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe kiliongezeka hadi asilimia 7.0 katika robo ya nne ya mwaka 2021 kutoka asilimia 0.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya almasi, chumvi, fedha, makaa ya mawe na gesi asilia. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa almasi uliongezeka hadi karati 34,430 mwaka 2021 kutoka karati 6,977 kipindi kama hicho mwaka 2020 na makaa ya mawe yaliongezeka hadi tani 346,009 mwaka 2021 kutoka tani 183,734 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2021

Madini	Kipimo	2016	2017	2018	2019	2020	2021
Gesi asilia	Mscf	12,257	13,075	15,872	16,760	16,447	17,494
Makaa ya Mawe	Tani	104,010	163,836	144,171	194,151	183,734	346,009
Madini ya Fedha	Tani	4,615	2,656	3,237	3,717	1,997	3,307
Chumvi	Tani	15,195	18,995	122,023	15,895	18,313	50,448
Almasi	Karati	32,410	80,540	121,436	76,995	6,977	34,430

Chanzo: Wizara ya Madini, 2021

2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.0 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.6 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inahusika na shughuli za usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozaishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali wa nishati ya umeme. Katika robo ya nne ya mwaka 2021, umeme uliosambazwa kwa wateja uliongezeka hadi saa za kilowati milioni 1,955 kutoka saa za kilowati milioni 1,768 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Shughuli ya uzalishaji umeme iliongezeka kwa kwa kiwango cha asilimia 10.6 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.9 kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.5 Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika robo ya nne ya mwaka 2021, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 96.4 kutoka mita za ujazo milioni 91.4 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kiliongezeka hadi asilimia 4.9 katika robo ya nne ya mwaka 2021 kutoka asilimia 3.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Sababu zilizochangia ongezeko hilo ni pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji wa maji.

Kielelezo Na. 7: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2021



Chanzo: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, 2021

2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli za ujenzi zinajumuisha, ujenzi wa nyumba za kuishi/makazi, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari, miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.5 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 5.2 ya kipindi kama hicho mwaka 2020. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika ujenzi. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo ni pamoja na chuma zilichangia ukuaji huo.

2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Shughuli hii pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo; na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Aidha, shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli za biashara na matengenezo ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 1.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa zikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo na bidhaa zilizozalishwa viwandani.

2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 1.2 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na

kiwango cha asilimia 8.9 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ultokana na ongezeko dogo la idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa katika kipindi hicho.

2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya malazi na huduma za chakula iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 11.3 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na kiwango hasi cha asilimia 14.9 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na ongezeko kubwa la watalii 298,296 walioingia nchini katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 190,528 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2020.

2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni; kurekodi sauti na kuchapisha muziki; shughuli za programu na utangazaji kwa mfano utangazaji wa redio na televisheni; mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya habari na mawasiliano kiliongezeka hadi asilimia 9.3 katika robo ya nne ya mwaka 2021 kutoka asilimia 7.0 katika robo ya nne ya mwaka 2020. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano Robo ya Nne, Mwaka 2019 – 2021

Kiashiria, kwa Robo Mwaka	2019	2020	2021
Muda wa maongezi (dakika milioni)	17,918	22,466	26,794
Ujumbe mfupi (milioni)	31,142	33,362	33,127
Wateja wa fedha kupitia mitandao ya simu ("000"), mwisho wa Desemba	25,864	32,269	35,286

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 2021

2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma za fedha na bima ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia 8.7 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli ya fedha na bima ilichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 14.4 kwa amana kutoka shilingi trilioni 23.1 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 26.4 mwaka 2021; kuongezeka kwa asilimia 10.5 kwa mikopo kutoka shilingi trilioni 19.8 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 21.9 mwaka 2021. Aidha, kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa asilimia 8.8 wa shughuli za bima mwaka 2021 kutoka asilimia 22.5 kipindi kama hicho mwaka 2020 kulichangia katika ukuaji wa shughuli hii.

Kielelezo Na. 8: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya nne, Mwaka 2016 – 2021



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2021

2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, na majengo; na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya upangishaji majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.5 mwaka 2021 kiwango sawa na ilivyokuwa kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundu na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli za kitaalam, kisanyansi na kiufundi iliongezeka hadi asilimia 6.2 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.2 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kuongezeka kwa huduma za kisheria na uhasibu katika shughuli hii kulichangia kiwango cha ukuaji uliofikiwa.

2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma zinazotolewa kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa huduma zinazohusiana na utawala kiliongezeka hadi asilimia 7.0 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.6 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii.

2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Ukuaji wa shughuli ya utawala na ulinzi uliimarika zaidi hadi asilimia 7.4 katika robo ya nne ya mwaka 2021 kutoka asilima 2.2 kipindi kama hicho mwaka 2020.

Kasi ya ukuaji ilitokana na ongezeko la matumizi ya fedha za Serikali kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama; pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali kupitia mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu inayotolewa kupitia sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.7 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

2.17 Afya

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine; na shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utaoji wa huduma za afya iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 katika robo ya nne ya mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 4.3 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma.

2.18 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya huduma nyingine za jamii iliendelea kuongezeka hadi asilimai 11.7 katika robo ya nne ya mwaka 2021 kutoka ukuaji wa asilimia 2.1 kipindi kama hicho mwaka 2020. Ongezeko la watalii na idadi ya watu katika maeneo ya mjini; na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za jamii kulichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

3.0 Hitimisho

Katika robo ya nne mwaka 2021, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.9 kutoka asilimia 4.8 kipindi kama hicho mwaka 2020. Shughuli ya huduma nyingine za jamii (ambayo inajumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri) ilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ukuaji wa asilimia 11.7; ikifuatiwa na huduma za chakula na malazi (asilimia 11.3); uzalishaji na usambazaji wa umeme (asilimia 10.6); habari na mawasiliano (asilimia 9.3); fedha na bima (asimia 8.7); utawala na ulinzi (asilimia 7.4); na uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 7.0).

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Nusu Mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biasara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393
2018		29,504,198	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,396,691	1,604,391	8,736,561	1,989,717	4,094,972
2019		30,802,027	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,802,021	10,965,038	1,645,950	9,493,191	2,133,312	4,281,167
2020		32,321,327	5,850,231	10,646,279	1,049,611	540,159	19,421,672	11,194,534	1,419,654	10,293,276	2,313,033	4,412,967
2013	1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
	2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
	3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
	4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
2014	1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
	2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
	3	4,450,294	929,381	1,788,128	213,998	97,099	2,228,708	2,035,245	361,470	1,686,150	414,058	960,721
	4	7,289,215	948,546	1,803,489	216,605	102,059	2,334,808	2,280,578	350,362	1,649,417	422,793	963,401
2015	1	6,605,887	923,326	1,733,636	211,828	96,862	2,438,046	2,093,973	346,778	1,654,599	386,446	995,846
	2	6,347,239	965,335	1,820,111	199,281	92,862	2,690,105	2,195,254	345,054	1,676,064	412,841	1,011,653
	3	4,656,388	960,427	1,939,664	192,215	99,585	2,601,253	2,162,776	372,080	1,764,202	441,478	1,076,143
	4	7,625,045	1,206,532	1,918,260	195,477	101,448	2,717,393	2,295,860	358,003	1,835,030	440,334	1,105,380
2016	1	6,788,342	1,017,609	1,965,656	214,850	95,779	2,859,933	2,295,506	358,142	1,818,390	401,047	1,111,056
	2	6,853,095	1,109,064	1,996,019	210,034	100,816	2,995,869	2,318,553	347,167	1,819,827	421,552	1,052,954
